Qiyaamu Ramadhaan

Na Imaam Muhammad
Naasir-ud-Deen Al-Albaanee

Asili: Qiyaamu Ramadhaan
Chapa ya Saba 1997/1417H
Imechapishwa na: Dar Ibn Hazm/Maktaba Islaamiyyah
Imefasiriwa kwa Kiswahili na: Abu Malaadh Sa'eed Baadel
Tarehe: Sept 2005 / Sha'aban 13, 1426H

Utangulizi wa Toleo la Pili

Sifa zote njema ni zenye kumthubutikia Allah, na neema na amani zimfikiye mtume wa Allah, familia yake, na maswahaba wake na wote wenye kufuata Sunnah. Ama baad:

Hii ni chapisho ya pili ya kijitabu changu "Qiyaamu Ramadhaan", ambacho nimewaleteeni wasomaji wakati huu karibu na kuandama mwezi mtukufu wa Ramadhaan, 1406H. Baada ya toleo la kwanza kuuzwa, na watu wengi kutaka kununua zaidi, nilitazama tena mas-ala haya na kufanya tarjuma na kuboresha kitabu hiki, pamoja na kuongeza midondoo ya hadeeth na maelezo zaidi yenye faida, ambayo nataraji yatamridhisha msomi, InshaAllah. Msomaji atona maelezo zaidi yenye faida katika sehemu ya 'Itikaaf.

Namwomba Allah, Aliyetukuka, kuniunganisha na hakki na kunisamehe kutokamana na yale nimekosea kwa kutofahamu kwangu na yalionipita ni kalamu yangu kutoweza kuyaandika. Namwomba Allah ajaaliye kitabu hiki kuwa nimeiandika kwa dhati ya kutaka Radhi zake, kwa hakika Yeye ni mwingi wa Msamaha, Mwenye Neema zote.

'Ammaan (Jordan)
Sha'baan 7, 1406H
Muhammad Naasir-ud-Deen Al-Albaanee

Utangulizi wa Toleo la Kwanza

Al-hamdu Lillaahi nasta'eenahu wa nastaghfiruhu, wa na'oodhu billaahi min shuroori anfusinaa wa sayi'aati a'maalinaa. Man yahdih Illaahu falaa mudilla lahu wa man yudlil falaa haadiya lahu. Wa ashhadu an laa ilaaha ill-Allaah wa ashhadu anna Muhammadan 'abduhu wa rasooluhu. Amma Baad:

Imepokewa kutoka kwa Ibn Mas'ood (radhiallahu anhu) kwa njia ya mawqoof, lakini inachukua hukmu ya marfoo' na kuwa ni kauli ya mtume, kuwa amesema:

كـــيف أنتم إذا لبستكم فتنة يهرم فيها الكبير ، ويربو فيها الصغير ، ويتخذها الناس سنة ، إذا منها شيء قيل : تركت السنة ؟ قالوا : ومتى ذاك ؟ قال : إذا ذهبت علماؤكم ، وكثرت قراؤكم ، وقلت فقهاؤكم ، وكثرت أمراؤكم ، وقلت أمناؤكم ، والتمست الدنيا بعمل الآخرة ، وتفقه لغير الدين

"Mutakuwaje itakapowafikieni fitnah kiwango ambacho barobaro atazeeka na kijana aenukie katika hali hio, na watu waifanye hio fitnah ndio kuwa sunnah? Kiasi cha kuwa sehemu ya hio itakapowachwa, watu watasema: "Umewacha kutekeleza Sunnah?"

Wakauliza: "Lini itafika hali hio?"

Akajibu:"Wakati wanavyuoni wenu wataaga dunia, wasomi watazidi, mafukahaa watapunguwa, viongozi watazidi, wanaodhaminika watapunguwa, anasa ya dunia itakimbiliwa kwa kufanya amali za akhera, na ilimu itatafutwa kwa sababu isiokuwa ya dini". [1]

Nami nasema: Hadeeth hii ni katika alama na ukweli wa utume wake (Salallahu Alaihi Wasallam), kwa hakika kila nukta ya hadeeth hii imeshatuhudhuria wakati huu. Miongoni mwake ni namna mambo ya bid'ah au uzushi inavyo enea kwa haraka, na watu kupewa mitihani na mambo haya, mpaka kufika kiwango kuwa watu wamechukulia kuwa ndio sunnah yenyewe inayostahiki kufuatwa. Ndio utakuta ya kwamba Ahlus-Sunnah wa kweli wanapojiepusha na kuyakemea mambo haya na kuelekea kwa sunnah ya halisi iliopokewa kwa bwana mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) watu wasema: "Jee wamewacha sunnah watu hawa?"

Hii ndio imetufikieni sisi Ahlu-Sunnah katika miji hizi za Shaam, tukihuisha sunnah ya kuswali taraweeh na raka'at kumi na moja, pamoja na kuzitekeleza kwa utulivu na khushui' na kutumia maneno saheeh katika adhkaar, kufanya kwa uwezo wetu. Hili ni jambo ambalo wengi wanao swali taraweeh kwa raka'at ishirini wamepungukiwa. Na juu ya haya, hasira zao na hamaki zilizidi tulipotoa kitabu chetu "Salaat-ut-Taraweeh", ambayo ni ya pili miongoni mwa vitabu vyingi tuliovitoa chini ya kitabu "Tasdeed-ul-Isaabah ilaa man za'ama Nusrat-al-Khulafaa ir-Raashideen was-Sahaabah". Yote yanatokamana na yale waliopata ndani yake kama:

1. Mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) mwenyewe hakuwahi kuswali taraweeh zaidi ya raka'at kumi na moja.

[1] Imepokewa na ad-Daarimee (1/64) na silsilah mbili ya wapokezi, moja ni saheeh na nyengine ni hasan. Pia imepokewa na al-Haakim (4/514) na wengineo.

2. 'Umar (radhiallahu anhu) alimuamrisha Ubay bin Ka'ab na Tameem ad-Daaree kuwaswalisha watu katika taraweeh raka'at kumi na moja kulingana na sunnah ilio saheeh.

3. Riwaya isemayo "Watu walikuwa wakiswali Qiyaamu Ramadhaan wakati wa Umar kwa raka'at ishirini" ni shaadh[2] na da'eef, ambayo inapinga riwaya ya juu yenye wapokezi wakutegemewa zaidi, ambao wametaja kuwa ni raka'at kumi na moja na kuwa 'Umar aliamrisha hayo.

4. Hata kama hadeeth hii ilio shaadh ni saheeh, ni aula zaidi kufuata kile kilicho saheeh yenye kuambatana na Sunnah tukitazama idadi ya raka'at. Pia hatuoni katika riwaya hio kuwa 'Umar aliamrisha watu kuswali rak'aat ishirini, bali watu tu walifanya hivo. Hii ni kinyume ya hadeeth ilio saheeh kuwa 'Umar aliamrisha raka'at kumi na moja.

5. Na hata kama riwaya hio ni saheeh haimaanishi kuwa watu wamelazimika kufuata hivo na kuacha kufuata riwaya nyengine ilio saheeh ambayo inaambatana na Sunnah, kufikia hadi kuwa mtu anapofuata Sunnah ahesabiwa kuwa ameenda kinyume na Jama'ah! Bali ni kinyume ya haya, kubwa tunaloweza kutoa katika hadeeth hii ni kuwa yaruhusiwa kuswali raka'at ishirini lakini iko wazi kuwa alichofanya mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) kila wakati ni raka'ah kumi na moja ambayo ndio bora.

6. Na pia tumeonesha kuwa kuswali raka'at ishirini haikuthibiti kuwa ni kitendo ya swahaba yeyote mtukufu miongoni mwao.

7. Na tukadhihirisha urongo wao wale wanaodai kuwa maswahaba wote waliafikiana kuwa ni raka'at ishirini.

8. Pia tukapambanua ushahidi wa kuwa mtu anatakikaniwa kufuata kile kilicho baini kutoka kwa Sunnah, na wale wanavyuoni waliopinga kuzidisha zaidi ya raka'ah hizo kumi na moja. Na haya pia yanahusu mas-ala mengine yenye faida tulioyataja ambayo ni nadra kupata yote yamekusanywa katika kitabu kimoja.

Nukta zote hizi zime-egezewa ushahidi ulio wazi katika sunnah ilio saheeh na hadeeth zinazo husiana nazo. Na hii ndio ilisababisha wajinga miongoni mwa wenye kufuata bendera tu kutukemea, wengine wao kwenye khutbah zao na darasa na wengine wameandika mpaka vitabu[3] ili kukemea kitabu chetu nilichokitaja hapa. Walakin, yote haya yamepungukiwa ilimu yenye manufaa wala hoja ya kuyathibitisha. Bali yamejaa matusi na jeuri tu, kama ilivyo ada ya warongo wanapopambana na ukweli na watu wake. Kwa ajili ya hayo, sioni faida ya sisi kupoteza wakati wetu kuwajibu na kudhihirisha makosa ya maneno yao. Hii ni kwa sababu maisha ni mafupi kuyapoteza na mambo haya, na twamwomba Allah awaongoze wote.

Lakini sioni ubaya kutaja mfano wa mmoja wao, ambaye nimemhisabu kuwa ni mwenye ilimu miongoni mwao.[4] Walakin, iwapo ilimu haiambatani na ikhlaas na tabia njema, itamletea mtu huyo hasara kuliko faida, kama alivyosema mtume (Salallahu Alaihi Wasallam)
"Mfano wa mtu anayefundisha watu mema na kuisahau nafsi yake ni mfano wa mshumaa, unatoa mwangaza lakini unajichoma na kumalizika".[5]

---

[2] Shaadh ni hadeeth ambayo imepokewa kutoka kwa mtu mwaminifu lakini yapingana na hadeeth nyengine ambayo ni yakutegemewa zaidi.

[3] Wamwisho wao ninayemkumbuka ni Muhammad 'Alee as-Saaboonee katika kitabu chake alichokiita "Uongozi Saheeh Wa Mtume kuhusu Salat Taraweeh". Tazama jawabu langu katika utangulizi wa mjao wa nne wa Silsilat-ul-Ahaadeeth As-Saheehah.

[4] Naye ni Shaikh Isma'eel Al-Ansaaree, mfanyi kazi katika ofisi ya Iftaa mjini Riyadh.

[5] Imepokewa na At-Tabaraanee na Ad-Diyaa Al-Maqdisee katika Al-Mukhtaar kutoka kwa Jundub na silsilah ya wapokezi ilio hasan. Pia tazama Saheeh At-Targheeb (1/56/127)

-- Imaam Al-Albaanee ametaja kirefu na kutoa mifano ya makosa ya mtu huyu. Walakin tumechagua kuepuka kipande hicho ili kuwaleteeni mlango wa kwanza wa kitabu hiki. --

Qiyaam katika Ramadhaan

Fadhila za kuswali salat at-Taraweeh katika mwezi wa Ramadhaan

1. Imesimuliwa katika ahadeeth mbili, yakwanza kutoka kwa Abu Hurairah, kuwa amesema:

عن أبي هريرة رضي الله عنه قال : كان رسول الله يُرَغبُ في قِيام رمضان ، من غير أن يأمرهم بعزيمة ، ثم يقول : من قام رمضان إيماناً واحتساباً غفر له ما تقدم من ذنبه فتوفي رسول الله والأمر على ذلك ، ثم كان الأمر على ذلك في خلافة أبي بكر رضي الله عنه ، وصدْر من خلافة عمر رضي الله عنه

"Mtume wa Allah (Salallahu Alaihi Wasallam) aliwahimiza kuswali swala ya usiku katika mwezi wa Ramadhaan, bila kutoa amri ya wazi. Kisha mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) alikuwa akisema:"Yeyote mwenye kusali swala ya usiku katika mwezi wa Ramadhaan huku akiwa na imani thabiti na kutarajia malipo, basi atasemehewa madhambi yake (madogo) yaliotangulia."

Basi mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) alifariki na jambo hili likabaki hali hio.[6] Ikaendelea kuwa hali hii wakati wa khilafa wa Abu Bakr (radhiallahu anhu) na sehemu katika khilaafa wa 'Umar (radhiallahu anhu).[7]

Hadeeth ya pili ni ile ya 'Amr bin Murrah al-Juhanee, ambaye alisema:

جاء رسول الله رجل من قضاعة فقال : يا رسول الله ! أرأيت إن شهدتُ أن لا إله إلا الله ، وأنــك رسول الله ، وصليتُ الصلوات الخمس ، وصمت الشهر ، وقمت رمضان ، وآتيتُ الزكاة ؟ فقال النبي من مات على هذا كان من الصديقين والشهداء

"Mtu kutoka Qudaa'ah alimjia mtume na kumwambia: "Ewe mtume wa Allah, wasemaje iwapo nitashuhudia kuwa hamna apasaye kuabudiwa kwa hakki ila Allah na kuwa wewe ni mjumbe Wake, na kisha niwe nitaswali swala tano za kila siku na nifunge na kuswali swala za usiku katika mwezi wa Ramadhaan, na nitowe Zakaat?" Mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) akasema: "Yeyote atakae kufa katika hali ya kutekeleza haya basi atakuwa ni miongoni mwa siddeeqeen[8] na mashahidi" [9]

---

[6] Kumaanisha kutoswali swalat Taraweeh kwa jamaah.

[7] Imepokewa na Muslim na wengineo na pia imepokewa na al-Bukhaaree hali ya marfoo' kutoka kwa mtume. Silsilah ya wapokezi imeelezwa kwa ubainifu katika Irwaa-ul-Ghaleel (4/14/906) na katika Saheeh Abu Dawood (1241). Namwomba Allah anisahilishie ili niweze kuichapisha. Ndugu Zuhair amesema katika maneno yake kwenye mdondoo juu ya kitabu changu "Swala za Eid mbili" (uk. 32), ambayo ilichapishwa tena mwaka 1404H: "Allah alisahilisha kuchapishwa kwa mjao wa kwanza wa Saheeh Abu Dawood ya mwalimu wetu al-Albaanee." Nami sielewi, kwa jina la Allah, vipi hii itawezekana ambapo mimi bado ninayo mjao wa kwanza na sikumruhusu mtu yeyote kutoa nakala yake, kando kuichapisha na kuisambaza! Pia mfano wa maneno haya ni aliyo yasema katika mjao wa nne wa kitabu changu at-Tawassul mwaka 1403H (uk 22) na mjao wa tatu wa Silsilat-ul-Ahadeeth ad-Da'eefah ilipochapishwa, ambapo hadi tarehe ya leo (Rajab ya 1406H) bado hakijachapishwa!

Laylatul Qadr na wakati wake:

2. Usiku ulio bora katika mwezi wa Ramadhaan ni ule wa Laylatul Qadr, kulingana na alivosema mtume (Salallahu Alaihi Wasallam):

من قام ليلة القدر (ثم وُفقتْ له) ، إيماناً واحتساباً ، غُفِرَ له ما تقدم من ذنبه

"Yeyote anayeswali swala ya Taraweeh usiku wa Laylatul Qadr [na kuipata] ilhali anayo imani thabiti na kutarajia malipo, atasamehewa dhambi zake ziliotangulia" [10]

3. Inapatikana usiku wa ishirini na saba katika mwezi wa Ramadhaan kulingana hoja yenye nguvu zaidi. Hadeeth nyingi inakubaliana na haya, ikiwemo ni hadeeth ya Zurr bin Hubaysh ambaye alisema:

زر بن حُبَيش قال : سمعت أُبيَّ ابن كعب يقول ـ وقيل له : إن عبد الله بن مسعود يقول : من قام السنة أصاب ليلة القدر ! ـ فقال أُبَيٌّ رضي الله عنه : رحمه الله ، أراد أن لا يتكل الناس ، والذي لا إله إلا هو ، إنها لفي رمضان - يحلف ما يستثني ووالله إني لأعلمُ أيّ ليلةٍ هي ؟ هي الليلة التي أمرنا رسول الله بقيامها هي ليلة صبيحة سبع وعشرين، وأمارتُها أن تطلع الشمس في صبيحة يومها بيضاء لا شعاع لها

"Nilimsikia Ubay bin Ka'ab (radhiallahu anhu) akisema wakati alipoambiwa kuwa 'Abdullah bin Mas'ood (radhiallahu anhu) amesema: "Yeyote anaye swali swala ya usiku mwaka mzima basi ataipata Laylatul Qadr". Yeye Ubay (bin Ka'ab) (radhiallahu anhu) akasema: "Mungu Amhurumie, nia yake nikuwa watu wasiwe (wavivu na) ni wenye kutegemea usiku huo pekee. Naapa kwa Yule ambaye hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki ila Yeye, usiku huo uko katika mwezi wa Ramadhaan tu. Na naapa kwa jina la Allah naijua inapatikana katika usiku gani. Ni usiku ambayo mtume wa Allah (Salallahu Alaihi Wasallam) alituamrisha kuswali Taraweeh. Nayo ni usiku wa ishirini na saba. Alama yake ni kuwa siku ya pili jua litapambazuka liking'aa bila ya kuwa na kengee."[11]

---

[8] Siddeeq ni hadhi wanaopewa wale wakwanza kuwaamini mitume na kustahamili ukweli wakati wa dhiki.

[9] Imepokewa na Ibn Khuzaimah na Ibn Hibban katika Saheeh zao, na wengineo, na silsilah ya wapokezi ilio saheeh. Tazama madondoo nilioandika katika Ibn Khuzaimah (3/240/2262) na Saheeh at-Targheeb (1/419/993).

[10] Imepokewa na al-Bukhaaree, Muslim na wengineo kupitia kwa Abu Hurairah (radhiallahu anhu) na Ahmad (5/318) kupitia kwa 'Ubaadah bin as-Saamit (radhiallahu anhu). Maneno ya ziada kwenye mabano [...] ni yake yeye na imepokewa na Muslim kupitia kwa Abu Hurairah. Neno muhimu: Katika mjao wa kwanza uliochapishwa wa kitabu hiki, nilikuwa nikitaja kiongezo katika sehemu ya mwisho ya hadeeth hii, yenye maneno haya "na dhambi zake za mbeleni" huku nikiegemeza mizani ya usahihi wa al-Mundhiree na al-'Asqalaanee. Kisha Allah akaniwezesha kuichunguza zaidi silsilah ya wapokezi wa hadeeth hii na yale yaliopokewa kupitia kwa Abu Hurairah na 'Ubaadah, ambapo sikuona mwengine mbele yangu kufanya hivo. Ndipo ikawa wazi kwangu kuwa kiongeza hiki "na dhambi zake za mbeleni" ni shaadh kutoka kwa Abu Hurairah na munkar (yenye kukataliwa) kutoka kwa 'Ubaadah. Kwa hivo nikafikia uamuzi kuwa wale walio kubaliana kuwa hadeeth ya Abu Hurairah kuwa ni hasan na ile ya 'Ubadah kuwa saheeh, kuwa uamuzi wao ni juu ya msimamo wao huu bila ya kuchunguza maneno haya. Nimeyataja haya kwa kirefu katika Silsilat-ul-Ahadeeth ad-Da'eefah (5083). Hii ndio sababu sikutaja kipande hicho cha hadeeth kutoka kwa Abu Hurairah nilipoitaja kwenye Saheeh at-Targheeb wat-Tarheeb (982), wala sikuitaja hadeeth ya 'Ubaada pamoja nayo, kinyume cha nilichofanya katika chapa ya asili ya at-Targheeb. Na Allah Aliyetukuka ndiye Mwenye kujaalia kufuzu.

[11] Imepokewa na Muslim na wengineo na nimeitaja katika Saheeh Aboo Dawood (1247)

Kusihi Kuswali swalat at-Taraweeh kwa Jama'ah

4. Kuswali swala ya Taraweeh kwa jama'ah imekubaliwa katika Sheria ya Kislamu. Bali ni bora zaidi kuliko mtu kuswali pekee yake kwa ajili mtume mwenyewe alilifanya jambo hili na pia kwa sababu ya kueleza kwake utukufu wa kuswali kwa jama'ah, kama inavopatikana katika hadeeth ya Abu Dharr (radhiallahu anhu) aliye sema:

أبي ذر رضي الله عنه قال : صمنا مع رسول الله رمضان ، فلم يقم بنا شيئاً من الشهر ، حتى بقي سَبْعٌ فقام بنا حتى ذهب ثلث الليل ، فلما كانت السادسة لم يقم بنا ، فلما كانت الخامسة قام بنا حتى ذهب شَطْرُ الليل ، فقلت : يا رسول الله! لو نَـفَّـلتنا قيام هذه الليلة ، فقال : إن الرجل إذا صلى مع الإمام حتى ينصرف حُسِبَ له قيام ليلة فلما كانت الرابعة لم يقم ، فلما كانت الثالثة جمع أهله ونساءه والناس ، فقام بنا حتى خشينا أن يفوتنا الفلاح . قال : قلت : ما الفلاح ؟ قال : السحور ، ثم لم يقم بنا بقية الشهر

"Tulifunga mwezi wa Ramadhaan na mtume wa Allah, lakini hakutuongoza katika swalah ya usiku katika mwezi wowote kabla hadi ilipobaki tu siku saba mwezi kumalizika, ndipo akatuongoza katika swalah hadi thuluthi ya usiku kupita. Ulipofika usiku wa sita, hakutongoza katika swalah ya taraweeh. Ulipofika usiku wa tano (yaani usiku wa 25) alituongoza tena katika swalah hadi nusu wa usiku kupita. Basi nikamuuliza: "Ewe mtume wa Allah! Jee tumalize sehemu ya usiku uliobaki tukiswali?" Naye akajibu: "Kwa hakika mtu anaposwali na imaam mpaka imaam akamaliza, atahesabiwa kuwa ameswali usiku mzima." Usiku wa nne hakutuswalisha taraweeh. Usiku wa tatu (yaani usiku wa 27) ulipofika,[12] yeye (Salallahu Alaihi Wasallam) aliwakusanya familia yake pamoja na wakeze na watu kwa jumla na kutuongoza katika taraweeh mpaka tukachelea kuwa tutaikosa falaah (kufuzu)". Nikauliza: "Nini hio falaah?". Naye (Abu Dharr) akajibu: "Ni Sahoor (chakula cha daku). Kisha mtume hakutuongoza tena katika swala siku ziliobakia."[13]

Sababu Mtume Kutoendeleza Salat ya Taraweeh kwa Jama'ah

5. Mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) aligoma kuswalisha Taraweeh kwa jama'ah siku zilizobakia wa mwezi wa Ramadhaan kwa sababu ya kuchelea isije swalah hio ikafanya kuwa ni faradhi kwa waislamu katika mwezi wa Ramadhani, na kuhofia ummah wasiweze kutekeleza jambo hilo. Hii imetajwa katika hadeeth ya A'isha ambayo inapatikana katika saheehain (Saheeh mbili yaani Bukhaari na Muslim) na zenginezo.[14] Lakini khofu hii ilikwisha mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) alipofariki, baada ya Allah kukamilisha sheria za Uislamu. Na kwasababu hii, ile khofu ya mtume iliyemsababisha kutoendeleza swalah ya taraweeh kwa jama'ah katika mwezi wa Ramadhaan pia imeondoka. Na ile hukmu yake ya mwanzo ya kukubaliwa swalah ya taraweeh kuswaliwa kwa jama'ah imebaki. Na hii ndio sababu Umar

[12] Hapa anamaanisha usiku wa 27 katika mwezi wa Ramadhaan, ambayo ndio Laylatul Qadar kulingana na rai ilio na nguvu zaidi, kama ilivyotajwa mbeleni. Hii ndio sababu ukaona katika usiku huu mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) aliwakusanya familia yake pamoja na wakeze. Kwa hivo hii ni hoja tosha kuwa imependekezwa wanawake kuhudhuria na kuswali kwa jamaah usiku huu.

[13] Hadeeth saheeh iliopokewa na maimaamu wote wa Sunan na wengineo. Nimeitaja na kuisahihisha katika Salaat-ut-Taraweeh (uk 16-17), na Saheeh Abu Dawood (1245), na Irwaa-ul-Ghaleel (447).

[14] Tazama maneno yenyewe na vidokezo vyake katika kitabu changu Salaat-ut-Taraweeh (uk 12-14)

(radhiallahu anhu) akaihuisha baadaye, kama ilivyo nukuliwa katika Saheeh Bukhaari na vitabu vyengine.[15]

Kusihi kwa Wanawake Kuswali Taraweeh kwa Jama'ah

6. Sheria imemruhusu mwanamke kuhudhuria na kuswali Taraweeh kwa jama'ah, kama ilivyotangulia katika hadeeth hapo mbeleni ya Abu Dharr. Isitoshe, inaruhusiwa kuwekwa imaam makhususan ili kuwaswalisha wanawake tu katika swalah hio kando na yule imaam anaye swalisha wanaume. Hii ni kwa sababu imepokewa katika hadeeth iliosihi kutoka kwa Umar (radhiallahu anhu) kuwa aliwakusanya watu kuswali taraweeh, akamchagua 'Ubay bin Ka'ab kuongoza wanaume na Sulaymaan bin Abee Hathma kuongoza wanawake. Arfajah ath-Thaqafee amenukuu:

كان علي بن أبي طالب رضي الله عنه يأمر الناس بقيام شهر رمضان ويجعل للرجال إماماً وللنساء إماماً ، قال : فكنت أنا إمام النساء

"Alee bin Abee Taalib (radhiallahu anhu) aliwaamrisha watu kuswali taraweeh mwezi wa Ramadhaan. Na aliwachagulia imaam mmoja kuwaongoza wanaume na mwengine wa wanawake. Nami nilikuwa imaam wa wanawake." [16]

Maoni yangu ni kuwa hii itafaa ikiwa msikiti ni mpana sana na inao nafasi kubwa ili kundi moja isiwe ni yenye kusumbuwa kundi la pili.

Idadi ya Rak'aat katika Qiyaam

7. Idadi ya rak'aat katika swala ya qiyaam ni kumi na moja, nasi twapendelea kuwa idadi hii isizidishwe au kuongezwa, ili kufuata sunnah na mwelekeo wa mtume (Salallahu Alaihi Wasallam), kwani kwa hakika yeye hakuenda zaidi ya idadi hii hadi alipofariki na kuaga dunia. 'Aisha (radhiallahu anha) aliulizwa kuhusu swalah ya mtume ya usiku wakati wa Ramadhaan na akajibu:

ما كان رسول الله يزيد في رمضان ولا في غيره على إحدى عشرة ركعة ، يصلي أربعاً فلا تسل عن حسنهن وطولهن ، ثم يصلي أربعاً فلا تسل عن حسنهن وطولهن ، ثم يصلي ثلاثا

"Mtume wa Allah hakuwahi kuswali zaidi ya rak'aah kumi na moja katika mwezi wa Ramadhaan au mwezi mwengine wowote. Alikuwa akiswali rak'aat nne, na musiniulize uzuri na urefu wa rak'aat hizo. Kisha aliswali tena rak'aat nne, tena musiniulizeni uzuri na urefu wa rak'aat hizo. Kisha aliswali rak'aat tatu."[17]

---

[15] Tazama vidokezo katika Ibn'Abdil-Barr na maneno ilivyokuja kwa njia nyengine katika kitabu Salaat-ut-taraweeh (uk 49-52)

[16] Hadeeth hii na ile iliotangulia zimepokewa na al-Bayhaqee (2/494). Yakwanza pia imepokewa na 'Abdur-Razzaq katika al-Musannaf (4/258/8722). Ibn Nasr pia ameipokea hadeethi hizi mbili katika Qiyaam Ramadhaan (uk 93) na kisha kuzitumia kuwa ni hoja kwa yale tulioyataja ukitazama (uk 95).

[17] Imepokewa na al-Bukhaaree, Muslim na wengineo, na nimeitaja katika Salaat-at-Taraweeh (20-21) na Saheeh Abu Dawood (1212)

8. Mtu anaweza kupunguza katika idadi hii apendavo hadi kufikia kiwango cha rak'a moja tu ya Witr. Hii imetegemezwa na ushahidi kutoka kwa vitendo na maneno ya mtume:

Ama kuhusu kitendo chake, 'Aisha aliulizwa ni rak'aat ngapi mtume alikuwa akiswali Witr, naye akajibu:

بكم كان رسول الله يوتر ؟ قالت كان يوتر بأربع وثلاثٍ ، وست وثلاثٍ ،
وعشر وثلاثٍ ، ولم يكن يوتر بأنقص من سبع ، ولا بأكثر من ثلاث عشرة

"Alikuwa akiswali witr kwanza kwa rak'aat nne[18] kisha tatu, pia kwa rak'aat sita kisha tatu, na kwa rak'aat kumi kisha tatu. Hakuwahi kuswali witr chini ya rak'aat saba wala zaidi ya kumi na tatu."[19]

Ama kuhusu kauli yake, mtume (Salallahu alaihi Wasallam) amesema:

الوتر حق ، فمن شاء فليوتر بخمس ، ومن شاء فليوتر بثلاث ، ومن شاء فليوتر لواحدة

"Witr ipo. Atakaye anaweza kuswali witr kwa rak'aah tano. Atakaye pia na aswali rak'aah tatu. Na atakaye pia na aswali witr kwa rak'a moja tu."[20]

Kisomo cha Qur'aan katika Qiyaam Layl

9. Kuhusu kusoma Qur'aan katika Qiyaamu-Layl mwezi wa Ramadhaan au miezi mengine, mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) hakuweka mipaka yeyote yakuwa mtu anaweza kuenda zaidi au chini yake. Kinyume yake, kisomo chake mwenyewe ilikuwa ikibadilika, mara huwa ni ndefu na mara nyengine fupi. Saa zengine utakuta akisoma urefu wa surah Muzammil, ambayo ina iyaat ishirini, kwa kila rak'ah. Na wakati mwengine akisoma urefu wa ayaat khamsini. Na alikuwa akisema:

من صلى في ليلة بمئة آية لم يُكتبْ من الغافلين

"Yeyote mwenye kuswali usiku na kusoma ayaat mia moja, hatoandikiwa kuwa ni miongoni mwa wale wenye kughafilika"

Na riwaya nyengine yasema:

بمئتي آية فإنه يكتب من القانتين المخلصين

"... na kusoma ayaat mia mbili, ataandikwa kuwa miongoni mwa wachamngu na wenye ikhlaas"

Usiku mmoja wakati mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) alikuwa mgonjwa alisoma zile sura saba ndefu, ambazo ni: al-Baqarah, Aali 'Imraan, an-Nisaa, al-Maidah, al-An'aam, al-A'raaf, na at-Tawbah.

---

[18] Nami nasema: Hii imekusanya zile rak'aat mbili za sunnah baada ya swala ya 'Ishaa au zile rak'aat mbili fupi ambayo mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) alikuwa akianzia swala ya Qiyaam. Na hii inatokamana na rai ya al-Haafidh Ibn Hajr. Tazama Salaat-ut-taraweeh (uk. 19-20)

[19] Imepokewa na Abu Dawood, Ahmad na wengineo. Silsilah ya wapokezi ni nzuri na al-'Iraaqee aliisahihisha. Nimeitaja katika Salaat-ut-taraweeh (uk 98-99) na Saheeh Abu Dawood (1233).

[20] Imepokewa na at-Tahawee, al-Haakim na wengineo. Silsilah ya wapokezi ni saheeh, kama ilivyokubaliwa na kundi la wanavyuoni. Pia inapatikana hadeeth nyengine yenye kuipa nguvu lakini hadeeth hio inayo kiongezeo ambayo imakataliwa kama nilivyoeleza katika Salaat-ut-Taraweeh (uk 99-100)

Na kwenye ile kisa cha Hudhaifah bin al-Yamaan wakati aliswali nyuma ya mtume swala moja ya usiku, yeye mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) alisoma katika rak'ah moja tu: Al-Baqarah, kisha an-Nisaa, kisha Aali Imraan. Na alikuwa akisoma taratibu pamoja na tilaawa. [21]

Na imesimuliwa pamoja na silsilah ya wapokezi ilio saheeh, kuwa 'Umar alimwaamrisha 'Ubay bin Ka'ab kuwaongoza watu kwenye swalah na raka'at kumi na moja katika mwezi wa Ramadhaan. Ubay alikuwa akisoma ma-mia ya ayaat mpaka kufikia hadi wale waliosali nyuma yake wakitemea mahali ili kujihimili kwa urefu wa kisimamo. Na hawakumaliza swalah ila karibu na kuingia alfajiri.[22]

Pia imepokewa kutoka kwa Umar kuwa aliwaita wanao-swalisha katika mwezi wa Ramadhaan na kuwaamrisha kuwa anayesoma kwa haraka na asoma ayaat thelathini, yule wa kati na asome ayaat ishirini na tano na yule anayesoma taratibu basi asome ayaat ishirini. [23]

Basi kulingana na haya, iwapo mtu ataswali Qiyaamu-Layl pekee yake basi aweza kuifanya ndefu apendavyo. Na hii pia ni sawa ikiwa kuna mtu anayeswali naye na akakubali kuwa arefushe. Kila mtu anapo refusha swalah basi hii ina fadhila zaidi, walakin, mtu asiruke mipaka kwa kurefusha swala mpaka kufikia kiwango wa kutumia usiku wote ilhali yumacho, isipokuwa nyakati nyengine tu, ili kufuata mwenendo wa mtume (Salallahu Alaihi Wasallam), aliyesema:

وخير الهدي هدي محمد

"Bora wa uwongofu ni uwongozi wa Muhammad"[24]

Wakati yeye alikuwa imaam, alikuwa akirefusha kiwango cha kutowatia dhiki na uzito wale walioko nyuma yake. Hii inatokamana na kauli yake mtume:

إذا قام أحدكم للناس فليخفف الصلاة ، فإن فيهم (الصغير) والكبير وفيهم الضعيف ، و (المريض) ، (وذا الحاجة) ، وإذا قام وحده فليطل صلاته ما شاء

"Mmoja wenu anapowaongoza wengine katika swala, basi aisahilishe swala, kwani miongoni mwao ni vijana, wazee, na miongoni mwa hao kunao wadhaifu, [wagonjwa][na wale wenye kutaka kutekeleza mahitaji yao]. Na akiwa ataswali pekee yake basi aweza refusha swala yake apendavo" [25]

Wakati wa Kuswali Qiyaamu katika Ramadhaan

10. Wakati wa swala ya Qiyaamu ni baada ya swalah ya 'Ishaa hadi wakati wa alfajiri. Na hii inatokamana na hadeeth ya mtume:

[21] Hadeeth zote hizi ni saheeh na nimezitaja katika Sifaat as-Salaat (uk 117-122)
[22] Hadeeth iliofanana nah ii imepokewa na Maalik. Tazama Salaat-ut-taraweeh (uk. 52)
[23] Tazama marejeo katika chimbuko iliotangulia (uk 71). 'Abdur-Razzaaq pia ameipokea katika al-Musannaf (4/261/479) vile vile al-Bayhaqee (2/497)
[24] Hii ni sehemu ya hadeeth iliopokelewa na Muslim, an-Nasaa'ee na wengineo. Nimeitaja katika Ahkaamul Janaa'iz (uk 18) na al-Irwaa (608).
[25] Imepokewa na al-Bukhaaree na Muslim. Riwaya hii iliotajwa hapa ni ya Muslim. Nimeitaja katika al-Irwaa (512) na Saheeh Abu Dawood (759 na 760)

إن الله زادكم صلاة ، وهي الوتر ، فصلوها بين صلاة العشاء إلى صلاة الفجر

"Kwa hakika, Allah amewaangozeni swala, nayo ni witr.[26] Kwa hivo iswalini baina ya 'Ishaa na swalah ya Fajr"[27]

11. Kuswali katika sehemu ya mwisho wa usiku ni bora kwa yule mwenye uwezo, kulingana na kauli ya mtume (Salallahu Alaihi Wasallam):

من خاف أن لا يقوم من آخر الليل فليوتر أوله، ومن طمع أن يقوم آخره فليوتر آخر الليل، فإن صلاة آخر الليل مشهودة وذلك أفضل

"Yeyote anayechelea kutoweza kuamka kuswali qiyaam sehemu ya mwisho ya usiku, basi na aiswali sehemu ya kwanza ya usiku. Na anayependa kuswali sehemu ya mwisho wa usiku basi na aifanye Witr sehemu ya mwisho ya usiku, kwa hakika kuswali sehemu ya mwisho ya usiku inashuhudiwa (na malaika), nayo ni bora."[28]

12. Iwapo mtu atakuwa na hiari ya kuswali sehemu ya kwanza pamoja na jama'ah na sehemu ya mwisho akiwa pekee yake, basi pamoja na jama'ah ni bora zaidi. Hii ni kwa sababu itahesabiwa kuwa ameswali usiku mzima, kama tulivyo taja katika nukta ya 4 ile hadeeth ilioenuliwa kuwa ni kauli ya mtume (Salallahu Alaihi Wasallam).

Maswahaba waliendelea kufanya hivi katika khilafa ya 'Umar (radhiallahu anhu). 'Abdur-Rahmaan bin 'Abdi al-Qaaree amehadithia:

فقال عبد الرحمن بن عبد القاري خرجت مع عمر بن الخطاب ليلة في رمضان إلى المسجد ، فإذا الناس أوزاع متفرقون ، يصلي الرجل لنفسه ، ويصلي الرجل فيصلي بصلاته الرهط ، فقال : والله إني لأرى لو جمعت هؤلاء على قارىء واحد لكان أمثل ، ثم عزم ، فجمعهم على أبيّ بن كعب ، قال : ثم خرجت معه ليلة أخرى ، والناس يصلون بصلاة قارئهم ، فقال عمر : نعمت البدعة هذه ، والتي ينامون عنها أفضل من التي يقومون - يريد اخر الليل - وكان الناس يقومون أوله

"Nilitoka na Umar bin al-Khattab usiku mmoja katika mwezi wa Ramadhaan kwenda msikitini, tulipowafikia kundi la watu waliotawanyika, mmoja alikuwa akiswali kando pekee yake na mwengine akiwasalisha kundi dogo nyuma yake. Basi yeye ('Umar) akasema: "Naapa kwa jina la Allah, naona iwapo nitawakusanya hawa watu wote pamoja wawe nyuma ya mtu mmoja akiwaswalisha, itakuwa ni bora zaidi." Basi akajikinaisha na haya na akawakusanya watu waswali nyuma ya Ubay bin Ka'ab. Baadaye siku nyengine nilitoka naye tena usiku na watu walikuwa wakiswali nyuma ya msomi mmoja. Naye 'Umar (radhiallahu anhu) akasema: "Hii ni jambo zuri niliolileta. Walakin wakati wanaolala ni bora kuliko wakati wanao swali sasa." -

[26] Swala yote ya usiku inaitwa Witr kwa sababu idadi ya raka'at inayoswaliwa ni witri [1,3,5,7 na kadhalika]
[27] Hadeeth saheeh ilopokelewa na Ahmad na wengine kutoka kwa Abu Basrah. Nimeitaja katika As-Saheehah (108) na al-Irwaa (2/158)
[28] Imepokewa na Muslim na wengineo. Nimeitaja katika as-Saheehah (2610)

kumaanisha sehemu ya mwisho ya usiku. Nao watu walikuwa wakiswali sehemu ya mwanzo ya usiku."[29]

Zayd bin Wahb amesema: **"Abdullaah alikuwa akituswalisha katika swalah wakati wa Ramadhaan, kisha akikoma inapokuwa usiku."** [30]

Namna ya Kuswali Qiyaamu katika Ramadhaan

Nimezungumza kirefu mas-ala haya katika kitabu changu Salaat-ut-taraweeh (uk 101-115), kwa hivo nikapendelea hapa nifupishe kwa mukhtasari ili iwe rahisi kueleweka kwa anayesoma pamoja na kumkumbusha:

Namna ya Kwanza: ni rak'aat kumi na tatu, ambayo inaanzia na raka'at mbili fupi. Kulingana na kauli ilio sawa zaidi ni kuwa hizi rak'aat mbili nizile za sunnah za baada ya 'Ishaa, au ni raka'at makhsusan ambazo mtu huanzia nayo Qiyaamu-Layl. Kisha mtu huswali raka'ah mbili ndefu baada yake. Kisha mbili zengine, tena na mbili zengine. Baadaye mbili zengine na fungu lengine la mbili. Kisha witr inamaliziwa na raka'ah moja.

Namna ya Pili: nayo ni raka'at kumi na tatu. Kunao raka'at nane ndani yake, ambapo mtu hutoa salamu baada ya kila raka'at mbili. Kisha witr inafanywa kwa raka'at tano na hukai wala kutoa salamu ila katika raka'ah ya mwisho ya tano.

Namna ya Tatu: nayo ni raka'at kumi na moja, ambayo utatoa salamu baada ya kila raka'at mbili kisha na kuswali witr kwa raka'ah moja.

Namna ya Nne: nayo ni raka'at kumi na moja, ambayo mtu ataswali raka'at nne kisha ndio atoe salamu moja tu baada ya nne. Kisha aswali tena nne kama mfano huu na kutoa salamu na kukamilisha na witr ya raka'at tatu.

Jee mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) atabaki katika kikao baada ya kila raka'at mbili, wakati anaposwali kitengo cha raka'ah nne au tatu? Hatupati jawabu iliowazi kueleza haya, lakini kubaki katika kikao (tashahhud) wakati wa kuswali witr ya raka'ah tatu imeharamishwa!

Namna ya Tano: itakuwa na raka'at kumi na moja, ambayo mtu ataswali raka'at nane ambayo hatobaki katika kikao ndani yake ila mwisho katika raka'ah ya nane. Anapokaa atafanya tashahhud na kutuma Salaat kwa mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) kisha atasimama bila kutoa salamu. Halafu ataswali witr raka'ah moja na kutoa salamu atakapo maliza. Hii itakuwa ni raka'at tisa. Kisha atakamilisha kwa kuswali raka'at mbili kwa kukaa.

Namna ya Sita: Ni kuswali raka'at tisa bila ya kukaa isipokuwa katika raka'ah ya sita. Kisha atafanya tashahhud na kumtumia Salaat mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) na baadaye atasimama bila kutoa salamu. Kisha ndio atafanya witr ya raka'at tatu na akimaliza ndio atatoa salamu. (iliobaki ni sawa kama ilivyotangulia)

Hizi ndio namna zilionukuliwa kuwa mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) aliswali Qiyaamu-Layl. Inawezekana kuongeza namna zengine juu yake, kwa mtu kupunguza anavyopenda katika kila

[29] Imepokewa na al-Bukhaaree na wengineo. Nimeitaja katika Salaat-ut-taraweeh (uk 48)

[30] Imepokewa na 'Abdur-Razzaaq (7741) pamoja na silsilah ya wapokezi ilio saheeh. Imaam Ahmad imeitaja hadeeth hii na ile iliotangulia kabla wakati alipoulizwa: "Swala ya Qiyaam, yaani taraweeh icheleweshwe hadi sehemu ya mwisho ya usiku?" Akajibu: "Laa, sunnah ya waislamu ni bora na yenye kupendekezwa zaidi kwangu mimi". Abu Dawood ameyapokea haya katika Masaa'il (uk 62).

kitengo cha raka'at mpaka kuikata na kubakia raka'ah moja, kufuata hadeeth iliotangulia ya mtume (Salallahu Alaihi Wasallam): **"Atakaye anaweza kuswali witr kwa rak'aah tano. Atakaye pia na aswali rak'aah tatu. Na atakaye pia na aswali witr kwa rak'a moja tu."** [31]

Iwapo mtu atataka aweza kuswali raka'at tano, au tatu na kikao kimoja na salamu, kama ilivyotajwa katika namna ya pili. Na akitaka aweza toa salamu baada ya kila raka'at mbili, kama vile namna ya tatu, na hii ndio imependekezwa.[32]

Ama kuswali raka'ah tano au tatu kisha mtu akae baada ya kila raka'at mbili bila kutoa salamu, basi hatukapata hata hadeethi moja ambayo ni saheeh kuwa mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) aliwahi kufanya hivo. Asili ya jambo kwa dini ni kuwa yaruhusiwa, walakin twakuta mtume (Salallahu Alaihi Wasalam) kutukataza kuswali witr kwa raka'at tatu na kutoa sababu kuwa:

ولا تشبهوا بصلاة المغرب

"Na musifananishe na swala ya Maghrib"[33] Hivyo basi mtu atakaye swali witr kwa raka'at tatu ni sharti asiifananishe na swala ya Maghrib. Hii inawezekana kwa njia mbili:

1. Kutoa salamu kati ya kifuasi na witri (yaani baina ya raka'ah ya pili na ya tatu). Hii ndio yenye nguvi na iliopendekezwa.

2. Mtu hakai katikati ya raka'ah (yaani ataswali zote tatu pamoja na kutoa salamu moja tu), na Allah Ndiye Mjuzi zaidi.

Kisomo ndani ya Raka'at tatu za Witr

14. Kuhusu raka'at tatu za witr, ni katika sunnah kusoma katika raka'ah ya kwanza: Sura Al-A'laa, katika raka'ah ya pili: Surah Al-Kaafiroon, na katika raka'ah ya tatu: Surah Al-Ikhlaas. Wakati mwengine mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) alikuwa akiongeza Surah Al-Falaq na An-Naas katika raka'ah ya tatu.

Pia imepokewa kutoka kwake (Salallahu Alaihi Wasallam) kuwa wakati mmoja alisoma ayaat mia kutoka kwa Surah An-Nisaa kwenye raka'ah ya tatu ya witr. [34]

Du'aa ya Qunoot na Pahala Pake

15. Baada ya kusoma na kabla ya kurukuu mtu saa zengine anaweza kuleta Qunoot hapa ambayo mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) alimfundisha mjukuu wake Hassan bin 'Alee (radhiallahu anhuma), nayo ni:

---

[31] Tazama nukta ya 8

[32] **Neno lenye faida**: Baada ya kutaja hadeeth ya 'Aisha na zengine kuhusu namna ya kuswali qiyaam katika Ramadhaan, Ibn Khuzaimah akasema katika Saheeh yake (2/194): "Kwa hivo inaruhusiwa kwa mtu kuswali raka'ah apendazo katika swalah ya usiku, kulingana na yale yaliopokelewa kutoka kwa mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) kuwa amefanya, pamoja na namna ilivopokewa kuwa amefanya mwenyewe. Hakuna aliyekatazwa kufanya yeyeto miongoni mwa haya." Na hii kauli, kutokamana na inavyo fahamika, inalingana kikamilifu na maoni yetu tulioshikilia na kupendekeza kuwa tushikamane na idadi iliopokewa kuwa mtume amefanya bila ya kuongeza chochote. Hivyo basi Sifa zote njema ni zenye kumthubutukia Allah kwa kutuwezesha haya na namwomba kutuzidishia katika Baraka zake.

[33] Imepokewa na at-Tahawee, ad-Daaraqutnee na wengineo. Tazama Salat-at-taraweeh (uk 99 na 110)

[34] Imepokewa na an-Nasaa'ee na Ahmad pamoja na silsilah ya wapokezi ilio saheeh.

اللهم اهدني فيمن هديت ، وعافني فيمن عافيت ، وتولني فيمن توليت ، وبارك لي فيما أعطيت ، وقني شر ما قضيت ، فإنك تقضي ولا يقضى عليك ، وإنه لا يذلّ من واليتَ ، ولا يعزّ من عاديت ، تباركت ربنا وتعاليت، لا منجا منك إلا إليك

Allahumm-ahdinii fiman hadait, wa 'afini fiman 'aafait, wa tawallani fiman tawwallait, wa barik li fima a'atait, wa qini sharra ma qadaiyta, fainnaka taqdhi wa la yuqdha 'alaika, innahu la yadhillu man walaiyt, [wa la yai'izzu man 'aadait] tabarakta Rabbana wa ta'aalaita [35]

Na mara nyengine ulete Salaat kwa mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) kulingana na yale tutakayo yataja baadaye.[36]

16. Hamna makosa kuleta Qunoot baada ya kurukuu, na kuongezea kwenye dua yenyewe kwa kuwalaani makafiri, kuleta Salaat kwa mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) na kuwaombea waislamu wote kwa jumla, katika nusu ya pili ya Ramadhaan kulingana na mfumo waliofuata maimaamu wakati wa 'Umar (radhiallahu anhu). Imetajwa katika sehemu ya mwisho wa hii hadeeth iliotajwa hapo awali ya 'Abdur-Rahmaan bin 'Abdin al-Qaaree:

"Nao waliwalaani makafiri katika nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhaan wakisema:

"Ewe Allah! Walaani makafiri wanao wapoteza watu kufuata njia Yako, wanaowakanusha mitume Wako na kutoamini Ahadi Yako. Watetanishe na ujaalie khofu ndani ya nyoyo zao. Na uwatumie adhabu kutoka Kwako, ewe Mola wa Hakki!"

Kisha yeye (imaam) atamtumia Salaat mtume (Salallahu Alaihi Wasallam), awaombee waislamu awezacho kuomba katika mambo ya kheiri, kisha amtake Mwenyezi Mungu msamaha wa waislamu."

Yeye ('Abdur-Rahmaan) kisha akasema: "Baada ya kuwalaani makafiri na kumtumia Salaat bwana mtume, kutaka msamaha kwa waumini na kuomba chochote kwa Allah, alikuwa akisema:

اللهم إياك نعبد ، ولك نصلي ونسجد ، وإليك نسعى ونحفد ، ونرجو رحمتك ربنا ، ونخاف عذابك الجد ، إن عذابك لمن عاديت مُلْحَقٌ

"Ewe Allah! Wewe ndio tunaekuabudu na Kwako Wewe tu ndio tunaswali na kusujudu, na ni Kwako tu tunakimbilia. Tunataraji Huruma kutoka kwako. Na tunaogopa adhabu yako ilio kali. Kwa hakika, adhabu yako huwafikia maadui Wako."

Kisha ataleta takbeer na kuenda katika sijdah.[37]

Kunasemwa Nini katika Sehemu ya Mwisho wa Witr

[35] Imepokewa na Abu Dawood, an-Nasaee na wengineo pamoja na silsilah ya wapokezi ilio saheeh. Tazama Sifat as-Salaat (uk 95 na 96 wa chapa ya 7)
[36] Tazama madondoo (notes) katika "Fadhila za kutuma Salamu kwa Mtume" (uk 33) na kifupisho cha kitabu Sifat as-Salaat an-Nabee (uk 45)
[37] Imepokewa na Ibn Khuzaimah katika Saheeh yake (2/155-156/1100)

17. Ni katika sunnah kusema katika sehemu ya mwisho wa Witr (kabla ya kutoa salaam au baada yake):

اللهم إني أعوذ برضاك من سخطك ، وبمعافاتك من عقوبتك، وأعوذ بك منك،
لا أحصي ثناءً عليك ، أنت كما أثنيت على نفسك

Allahumma inni a'udhubika bi ridhaaka min sakhatika, wa bi mu'aa-faatika min 'uqubatika, wa a'udhubika minka, la uhsi thana'an 'alaika, anta Kama athnayta 'ala nafsika[38]

18. Na unapotoa salamu kumaliza swala ya witr inatakiwa kusema: "Subhaan al-Malik al-Qudoos, Subhaan al-Malik al-Qudoos, Subhaan al-Malik al-Qudoos, na kurefusha pamoja na kuenua sauti unapoisema mara ya tatu.[39]

Raka'at Inayofuatia

19. Unaweza kuswali raka'at mbili baada ya haya, kulingana na kauli sahihi kutoka kwa mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) kuwa amefanya hivo.[40] Ama kwa hakika, aliamrisha umma kuongeza hizi raka'at mbili, kwani alisema:

إن هذا السفر جهد وثقل ، فإذا أوتر أحدكم ، فليركع ركعتين ، فإن استيقظ وإلا كانتا له

"Hakika safari aina hii ni ya juhudi na mzigo, hivyo basi mmoja wenu atakaposwali Witr basi mwacheni aongeza raka'at mbili baada yake. Basi iwapo ataamka au laa, itakuwa ashaandikiwa."[41]

20. Sunnah nikusoma Surah az-Zilzaal na al-Kaafiroon katika raka'ah mbili hizi.[42]

'ITIKAAF

Amri Yake

1. 'Itikaaf ni jambo liliopendekezwa wakati wa Ramadhaan na wakati wowote mwengine katika mwaka. Asili yake inatokamana na ayaah ya Allah aliposema: **"....wakati munafanya 'itikaaf kwenye misikiti."** Pia kunapatikana hadeeth nyingi zilizo saheeh kuhusu 'itikaaf ya mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) na pia misemo kutoka ma Salaf kuhusu maudhui haya ambayo yametajwa katika Musannafs ya Ibn Abee Shaybah na 'Abdur-Razzaaq. [43]

---

[38] Saheeh Abu Dawood (1282) na al-Irwaa (430)

[39] Saheeh Abu Dawood (1284)

[40] Imepokewa na Muslim na wengineo. Tazama Salaat-at-taraweeh (uk 108-109)

[41] Imepokewa na Ibn Khuzaimah katika Saheeh yake, ad-Daarimee na wengineo. Nimeitaja katika As-Saheehah. Ilikuwa nikichelea katika kutekeleza raka'at hizi kwa muda. Lakini kisha niliposoma hii amri ya mtume (Salallahu Alaihi Wasallam), nikashikamana nayo na kuitekeleza. Na nikatambua kuwa mtume aliposema **"Fanyeni swalah yenu ya mwisho kuwa ni witiri"** hii ni amri ya kupendekeza wala sio amri ya kulazimu. Na hii pia ndio rai ya Ibn Nasr (130).

[42] Imepokewa na Ibn Khuzaimah (1104-1105) kutoka kwa hadeeth ya 'Aisha na Anas, Allah awaridhie, na silsilah mbili za wapokezi zikitiana nguvu. Tazama Sifat Salaat an-Nabee (uk 24)

[43] Katika chapa iliopita ya kitabu hiki, hapa kulikuwa na hadeeth kuhusu "Yeyote mwenye kufanya 'Itikaaf siku moja ...", lakini nimeondoa sasa baada kupeleleza kuwa ni dhaeef. Hii ni baada ya kutazama kwa makini na kuizungumzia kwa kirefu katika Silsilatul-Ahaadeeth ad-Daeefah (5247). Huko utaona nimeonesha udhaeefu wake ambayo ilikuwa sikujua mbeleni na hata Al-Haythaamee kabla yangu pia ilimpita!

Imenukuliwa kuwa mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) alifanya 'Itikaaf katika kumi la mwisho wa mwezi wa Shawaal, [44] na 'Umar (radhiallahu anhu) alimuuliza mtume (Salallahu Alaihi Wasallam):

كنت نذرت في الجاهلية أن أعتكف ليلة في المسجد الحرام ؟قال :
فأوف بنذرك ، (فاعتكف ليلة)

"Siku moja wakati wa Jahiliyyah niliapa kuwa nitafanya 'Itikaaf usiku mmoja katika Masjid al-Haraam, (jee nitekeleze?)", Mtume akamjibu: "Tekeleza kiapo chako." Basi akafanya 'Itikaaf usiku mmoja."[45]

2. Kuifanya katika mwezi wa Ramadhaan inapatikana katika hadeeth ya Abu Hurairah:

كان رسول الله يعتكف في كل رمضان عشرة أيام ،
فلما كان العام الذي قبضَ فيه اعتكف عشرين يوما

"Mtume wa Allah alikuwa akifanya 'Itikaaf siku kumi kila Ramadhaan. Lakini mwaka wake wa mwisho alipofariki, alifanya 'Itikaaf siku ishirini."[46]

3. Wakati bora kuifanya ni sehemu ya mwisho ya Ramadhaan kwa sababu mtume (Salallahu Alaihi Wasallam)

كان يعتكف العشر الأواخر من رمضان حتى توفاه الله عز وجل

alifanya 'Itikaaf kila siku kumi za mwisho wa Ramaadhan mpaka Allah alipoichukua roho yake. [47]

Masharti Yake:

1. Imeeandikiwa isifanywe popote illa kwenye misikiti, kulingana na ayaah ya Allah:

وَلَا تُبَٰشِرُوهُنَّ وَأَنتُمۡ عَٰكِفُونَ فِي ٱلۡمَسَٰجِدِۗ

"Na wala musiwaingilie (wake zenu) ilhali muko katika 'Itikaaf misikitini" [Surah al-Baqarah : 187][48]

Na 'Aisha amesema:

---

[44] Hii ni sehemu ya hadeeth ya 'Aisha iliopekewa na al-Bukhaaree, Muslim, na Ibn Khuzaimah katika vitabu vyao. Nimeitaja katika Saheeh Abu Dawood (2127).

[45] Imepokewa na al-Bukhaaree, Muslim, na Ibn Khuzaimah. Maneno ya ziada ni kutoka kwa al-Bukhaaree katika riwaya moja kama nilivotaja katika ufupisho wangu (995). Na nimeitaja vile vile katika Saheeh Abu Dawood (2136-2137).

[46] Imepokewa na al-Bukhaaree na Ibn Khuzaimah katika saheeh zao, na nimeitaja kama ilivyokuja kwenye nukta ya juu (2126-2130).

[47] Imepokewa na al-Bukhaaree na Muslim na Ibn Khuzaimah (2223) na nimeitaja katika al-Irwaa(996) na Saheeh Abu Dawood (2125).

[48] Imaam al-Bukhaaree alitumia ayaah hii kama ushahidi wa yale tuliotaja hapo juu. Al-Haafidh Ibn Hajr akasema: "Ushahidi unaopatikana kwa ayaah hii ni kuwa iwapo ni sawa kufanya 'Itikaaf mahala pengine isipokuwa misikitini basi kukatazwa kwa kuingiliana na wake isingetajwa, kwa sababu kuingiliana kumekatazwa wakati wa 'Itikaaf kulingana na rai ya wanavyuoni wote. Hivyo basi yaeleweka kuwa kutajwa hapa neno "misikiti" ni kuwa 'Itikaaf haikubaliwi isipokuwa ndani ya misikiti.

السنة في المعتكف أن لا يخرج إلا لحاجته التي لا بد له منها ، ولا يعود مريضاً ، ولا يمس امرأته ، ولا يباشرها ، ولا اعتكاف إلا في مسجد جماعة ، والسنة فيمن اعتكف أن يصوم

"Sunnah kwa yule anayefanya 'Itikaaf ni kuwa asitoke nje ya msikiti isipokuwa kwa dharura. Asifuate mazishi yeyote, wala asipumzike na mkewe wala kuingiliana naye. Na hamna 'Itikaaf isipokuwa iwe ndani ya msikiti ambayo haiswaliwi jama'ah. Na vile vile sunnah kwa yule afanyae 'Itikaaf kuwa afunge siku hio."[49]

2. Sharti msikiti uwe pia waswaliwa swalah ya Ijumaa ili mtu asifaradhike kutoka ili kuenda kuswali Ijumaa kwengine. Kwa sababu kutoka ili kuswali Ijumaa ni faradhi, kulingana na moja ya riwaya ya 'Aisha ya hadeeth iliotangulia ni:

...ولا اعتكاف إلا في مسجد جامع

" ... na hamna 'Itikaaf isipokuwa kwa msikiti wenye kuwa na swalah ya Ijumaa."[50]

Ikizidi, nimepata hadeeth saheeh ilio wazi kabisa yenye kutaja "misikiti" iliokusudiwa haswa katika ayaah iliotangulia kumaanisha misikiti mitatu: Masjid Al-Haraam, Masjid an-Nabawee, na Masjid al-Aqsa.

Hadeeth yenyewe ni:

لا اعتكاف إلا في المساجد الثلاثة

"Hamna 'Itikaaf isipokuwa kwa misikiti mitatu"[51]

Kulingana na nilioyapitia, miongoni mwa Salaf wenye kuwa na rai hii ni Hudhayfah Ibn Al-Yamaan, Sa'eed Ibn Al-Musayyib na 'Ataa. Walakin, yeye ('Ataa) hakutaja msikiti wa al-Aqsaa. Wengine walikuwa na maoni kuwa ni msikiti wowote wenye kuswaliwa Ijumaa bila kuweka mkazo wowote. Na wengine wamepinga pia haya na kusema yaweza kuwa hata kwa msikiti wa mtu nyumbani. Na hamna shaka kuwa kufuata yale yanaokubaliana na hadeeth ndio inayopaswa na kuwa na hakki zaidi kufuatwa. Na Allah Aliyetukuka ndio Mjuzi zaidi.

3. Ni katika sunnah kwa anayefanya 'Itikaaf kufunga, kama ilivyotajwa na 'Aisha (radhiallahu anha).[52]

---

[49] Imepokewa na al-Bayhaqee na silsilah ilio saheeh, na kutoka Abu Dawood ni silsilah nzuri. Riwaya hii ya 'Aisha pia yatoka kwa Abu Dawood, na nimeitaja katika Saheeh Abu Dawood (2135) na al-Irwaa (966)

[50] Al-Bayhaqee amepokea kuwa Ibn 'Abbaas (radhiallahu anhu) amesema: "Kwa hakika, vitu vichukiavyo zaidi kwa Allah ni vitu vya bid'ah (uzushi). Na kwa hakika moja katika bid'ah ni kufanya 'Itikaaf ndani ya misikiti ilioko ndani ya majumba."

[51] Imepokewa na at-Tahawee na al-Isma'eelee na al-Bayhaqee na silsilah ya wapokezi ilio sahihi kutoka kwa Hudhaifa bin Al-Yamman. Na nimeitaja katika As-Saheehah (2786) pamoja na riwaya kutoka maswahaba wengine inayolingana na hii, na riwaya zote hizo ni saheeh.

[52] Imepokewa na Al-Bayhaqee na silsilah ya wapokezi ilio saheeh na Abu Dawood yenye silsilah ambayo ni hasan. Imaam Ibn Al-Qayyim asema katika Zaad al-Ma'aad: "Haikupokewa kutoka kwa mtume kuwa aliwahi kufanya 'itikaaf bila kufunga." Na isitoshe, Allah hakuitaja 'Itikaaf ila pamoja na saum. Na mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) hakufanya ila wakati alifunga. Hivyo basi maoni ilio saheeh iko kwenye ushahidi, ambayo wanavyuoni wengi wameafikiana kuwa: kufunga ni sharti ya kufanya 'Itikaaf. Na hii ndio rai ya Shaikh-ul-Islaam Abul-'Abbaas Ibn Taymiyyah. Naye akaongezea kuwa hakuna mahali kwenye sheria kuwa mtu atatoka kuelekea msikitini kuswali au kufanya jambo lolote lile na huku aweke nia ya kiwango cha wakati atakayo tumia akiwa kwenye 'Itikaaf. Hivi ndio Shaikh-ul-Islaam ametaja katika Ikhtiyaaraat.

Kitu Gani kinaruhusiwa Ndani ya 'Itikaaf

1. Anaruhusiwa kutoka nje ili kutekeleza dharura fulani. Pia anaruhusiwa kutoa kichwa chake nje ili kioshwe na kuchanwa. 'Aisha (radhiallahu anha) amesema:

وإن كان رسول الله ليدخل عليّ رأسه وهو (معتكف) في المسجد ، (وأنا في حجرتي) فأرَجِّلُهُ ، (وفي رواية : فأغسله وإن بيني وبينه لعتبة الباب وأنا حائض) ، وكان لا يدخل البيت إلا لحاجة (الإنسان) ، إذا كان معتكفاً

"Mtume wa Allah aliingiza kichwa chake kwangu ilhali yeye alikuwa akifanya 'Itikaaf nami niko ndani ya chumba changu. Basi nikimchana [na katika riwaya nyengine: nikimwosha kichwa chake japokuwa kulikuwa na nafasi baina yangu na yeye, nami nilikuwa katika damu ya hedhi naye mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) hatoingia nyumbani ila kwa dharura wakati anapofanya 'Itikaaf"[53]

2. Anaruhusiwa mwenye kufanya 'Itikaaf na wengine kutawadha wakiwa msikitini, kulingana na ile hadeeth ya yule mtu aliekuwa akimhudumia mtume **"mtume alikuwa akitawadha akiwa msikitini"** [54]

3. Anaruhusiwa kutenga mahali na kuweka hema sehemu ya nyuma ya msikiti ili kukaa 'Itikaaf. Hii ni kwa sababu 'Aisha (radhiallahu anha) alikuwa akimwekea khibaa[55] (hema) mtume naye alikuwa akifanya 'Itikaaf. Na hii ni katika amri yake mtume (Salallahu Alaihi Wasallam).[56]
Na wakati mmoja alifanya 'Itikaaf katika hema dogo[57] ambalo lilikuwa na mkeka mdogo wenye kuziba nafasi ya mahala pa kuingilia.[58]

Ruhusa ya Mwanamke kufanya 'Itikaaf na kumtembelea mume wake msikitini

4. Inaruhusiwa kwa mwanamke kumtembelea mumewe anayekaa katika 'Itikaaf. Na anaweza kutembea naye hadi mlangoni wakati wa kumuaga kulingana na ushahidi wa hadeeth ya Safiyyah (radhiallahu anha):

---

[53] Imepokewa na al-Bukhaaree, Muslim, Ibn Abee Shaybah, na Ahmad na kiongezi cha kwanza kwenye hadeeth ni ya hawa wawili niliowataja mwisho. Nimeitaja katika Saheeh Abu Dawood (2131-2132)

[54] Imepokewa na Al-Bayhaqee na silsilah ya wapokezi ambayo ni hasan, na Ahmad (5/364) kwa ufupi yenye silsilah ilio saheeh.

[55] Khibaa ni aina ya hema waarabu walikuwa wakitengeza kutokamana na pamba au manyoya, na si kutoka manyoya ya wanyama na husimamishwa kwa milingoti miwili au mitatu. Tazama An-Nihaayah.

[56] Imepokewa na Al-Bukhaaree na Muslim kutoka kwa hadeeth ya 'Aisha. Kitendo chake ni kutoka kwa hadeeth ya Bukhaaree na maamrisho yake kutoka katika riwaya ya Muslim.

[57] Suddah kwenye hema ni kama kizibio kwenye mlango ili kukinga maji ya mvua kuingia. Kinacho maanishwa hapa ni kuwa kipande cha mkeka kimewekwa ili watu wasiweze kuchungulia ndani. Al-Sindee ndio ametaja hivo. Lakini ni bora kusema: Ili hali ya yule aliye kwenye 'Itikaaf isisumbuliwe na kujishughulisha na wale wanaopita mbele yake, ili apate kutekeleza malengo ya kukaa 'Itikaaf. Hivi ndio Imaam Ibn Al-Qayyim alivyosema: "Hii ni kinyume na vile mtu mjinga anavyofanya ambaye utamwona anapafanya mahala pake pa 'Itikaaf kuwa ndio mahala pa urafiki, na kupokea wageni na kusungumzia sehemu za hadeeth. Kwa hivyo hii ni aina moja ya 'Itikaaf na 'Itikaaf ya mtume ni aina nyengine."

[58] Ni sehemu ya hadeeth iliyosimuliwa na Abu Sa'eed Al-Khudree, na kupokewa na Muslim na Ibn Khuzaimah katika saheeh zao. Nimeitaja katika Saheeh Abu Dawood (1251)

كان النبي معتكفاً (في المسجد في العشر الأواخر من رمضان) فأتيته أزوره
ليلاً ، (وعنده أزواجه ، فرُحْنَ) ، فحدثتُهُ (ساعةً) ، ثم قمت لأنقلبَ ، (فقال :
لا تعجلي حتى أنصرف معك) ، فقام معي ليقلبني ، وكان مسكنها في دار
أسامة بن زيد (حتى إذا كان عند باب المسجد الذي عند باب أم سلمة) ، فمر
رجلان من الأنصار ، فلما رأيا النبي أسرعا ، فقال النبي : على رسلكما ؛
إنها صفية بنت حيي ، فقالا : سبحان الله ! يا رسول الله ! قال : إن الشيطان
يجري من الإنسان مجرى الدم ، وإني خشيتُ أن يقذف في قلوبكما شراً ، أو قال : شيئاً

"Mtume alikuwa akikaa 'Itikaaf msikitini katika kumi la mwisho la Ramadhaan, basi nikaenda kumtembelea usiku mmoja, wakati wakeze wengine walikuwa naye. Basi nikasema naye kama muda wa saa, kisha nikasimama kutoka naye akasema : "Usiwe na haraka, nitakusindikiza". Akasimama na kunisindikiza nje." Na makazi yake ilikuwa ni nyumba ya Usamah bin Zaid. Basi wakatembea hadi kufika mlango wa msikiti ambayo ilikuwa karibu na mlango wa Umm Salamah. Basi watu wawili waki-Ansaar walikuwa wakipita na walipomuona mtume waliondoka kwa upesi. Basi mtume akasema:"Musifanye haraka! Huyu ni mke wangu Safiyyah bint Huyai" Wakasema: SubhaanAllah, Ewe mtume wa Allah". Akasema: "Kwa hakika shetani yuwatembea ndani ya binadamu kama vile damu. Nami nilihofia asije kuwatia dhana mbaya kwenye nyoyo zenu." [au alisema: "kitu ndani ya nyoyo zenu"][59]

Mwanamke anaruhusiwa pia kukaa 'Itikaaf pamoja na mumewe msikitini au pekee yake, kulingana na hadeeth ya 'Aisha (radhiallahu anha)

اعتكفتْ مع رسول الله امرأة مستحاضة (وفي رواية أنها أم سلمة) من أزواجه ، فكانت
ترى الحمرة والصفرة ، فربما وضعنا الطَّسْتَ تحتها وهي تصلي

"Mmoja katika wakeze mtume (Salallahu Alaihi Wasallam) alikaa 'Itikaaf naye ilhali alikuwa na istihaadha (damu itokao baada ya hedhi) [na katika riwaya nyengine yasema alikuwa ni Umm Salamah] na alikuwa akiona mtiririko mwekundu au manjano (ukimtoka). Na saa zengine tulikuwa tukiweka sahani chini yake anaposwali."[60]

Na pia alisema:

كان النبي يعتكف العشر الأواخر من رمضان حتى توفاه الله،ثم اعتكف
أزواجه من بعده

"Mtume alikuwa akikaa 'Itikaaf katika kumi la mwisho la Ramadhaan, mpka kufariki kwake. Na wakeze walikaa 'Itikaaf baada ya kuondoka kwake." [61]

Kuna ushahidi kutoka maneno haya kuwa inaruhusiwa mwanamke kukaa 'Itikaaf vile vile. Na hamna shaka kuwa sharti wapewe ruhusa na wasimamizi wao. Na pia iwe ni hali ambayo hakutapatikana fitnah na kuchanganyikana na wanaume, kutokamana na hadeeth nyingi yenye

[59] Imepokewa na Al-Bukhaaree na Muslim na Abu Dawood, na sehemu ya mwisho yatoka kwake (Abu Dawood). Na nimeitaja katika Saheeh Abu Dawood (2133 na 2134)
[60] Imepokewa na Al-Bukhaaree na nimeitaja katika Saheeh Abu Dawood (2138). Riwaya nyengine inatoka kwa Sa'eed Ibn Mansoor, kama ilivyotajwa katika Fath-ul-Baaree (4/281). Walakin, Ad-Daarimee (1/22) asema kuwa ni Zaynab, na Allah ndiye Mjuzi zaidi.
[61] Imepokewa na Al-Bukhaaree, Muslim na wengineo.

kupinga hayo, na pia kulingana na asili ya fiqh kuwa : "kuepusha dhambi kufanyika huchukua nafasi ya mbele kuliko kufanya jema"

5. Kuingiliana mume na mke huvunja 'Itikaaf, ushahidi kutoka ayaah ya Allah:

Ibn 'Abbaas (radhiallahu anhu) asema:"Ikiwa mtu amekaa 'Itikaaf na akaingiliana na mkewe basi atakuwa amevunja 'Itikaaf yake na lazima aenze tena upya." [62] Hamna kafaara yeyote inayotakikaniwa kwa mwenye kufanya haya kwa sababu hatukupata chechote kutoka kwa mtume au maswahaba wake yenye kuashiria haya.

"Subhaanak Allah wabihamdika. Laa ilaaha ila anta, nastaghfiruka wanatoobu ilaik"

Hii itakamilisha maregeo haya, viongezi na maneno zaidi yenye faida yalioandikwa hapa na mtungaji, wakati ni al-Fajiri, Ijumapili tarehe 26 mwezi wa Rajab, 1406H. Namwomba Allah atume Salaat na Salamu kwa mtume wake Muhammad, mtume asiyeweza kusoma na kuandika, na familia yake na maswahaba wake.

'Amaan, Jordan
Muhammad Naasir-ud-Deen Al-Albaanee

[62] Imepokewa na Ibn Abee Shaybah (3/92) na 'Abdur-Razaaq (4/363) na silisilah ya wapokezi ilio saheeh. Anachomaanisha katika msemo wake "lazima aanze tena upya" ni kuwa lazima arudie tena 'Itikaaf.